Jarida la DCEA
TOLEO LA TATU 2023/2024
ISSN NO. 978 - 9912 - 9896 - 1 - 0

# DAWA ZA KULEVYA

Kataa Dawa za Kulevya, Timiza Malengo Yako

HALIUZWI



## Wazazi Fuatilieni Mienendo ya Watoto Wenu

- Rais Dkt. Samia

**Uk. 3&5**
Aretas Lyimo Hapoi Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

**Uk. 8&9**
Mali za Mfanyabiashara wa Dawa za Kulevya Zataifishwa

**Uk. 12&13**
'Sigara ya mpenzi iliniponza, nikaishia katika utumwa wa unga'

**Uk. 20**
Ijue Maana ya Nembo Mpya ya DCEA








## Yaliyomo


'Wazazi Fuatilieni Mienendo ya Watoto Wenu' - Rais Dkt. Samia >>>




Uk.2

Aretas Lyimo Hapoi Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya >>>



Uk.3&5

DCEA, TAKUKURU Zaunganisha Nguvu Kupinga Rushwa na Dawa za Kulevya >>> Uk.6&7





Matukio Pichani >>> Uk.10&11

'Tumeamua kubadilika, familia, jamii msitutenge' - Brown >>>



Uk.13

Wapelelezi na Waendesha Mashtaka wa Serikali Wajengewa Uwezo >>>



Uk.20

Katuni >>> Uk.21&22

Tahariri

# Nafasi ya Malezi Katika Kuikinga Jamii na Dawa za Kulevya



*UTUMIAJI wa dawa za kulevya miongoni mwa vijana hutofautiana kati ya nchi na nchi. Kwa upande mmoja, dawa ya kulevya hutumiwa katika mazingira ya burudani ili kuongeza msisimko. Kwa upande mwingine, vijana wanaopitia changamoto za kimaisha hutumia dawa ya kulevya wakidhani ni njia sahihi ya kukabiliana na changamoto hizo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya Mwaka 2018, Watoto na vijana hujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kutokana na matatizo ya afya ya akili, vinasaba, ushawishi wa kijamii, malezi ya wazazi, shule na msukumo rika, pamoja na mazingira ya kijami.*

*Kutokana na sababu zilizotajwa, suala la malezi ni nguzo muhimu sana katika kuikinga jamii dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwani hujenga msingi imara kwa watoto na vijana na kuwapa uwezo wa kuchanganua mambo na kujiepusha na vitendo viovu ikiwemo kutumia dawa za kulevya.*

*Hivyo basi, wazazi na walezi wanapaswa kuwa kioo au mfano bora kwa watoto wao kwa kuonesha tabia na maadili yanayofaa.*

*Tafiti ya Rachel N. Lipari ya **"Watoto wanaoishi na wazazi walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya"** inaonyesha kwamba, watoto ambao wazazi wao hutumia dawa za kulevya wanakabiliwa na changamoto ya unyanyasaji. Aidha, tafiti hiyo inaongeza kuwa matumizi ya vilevi hupelekea wazazi kutokekeleza majukumu yao, na watoto wanaweza kuathiriwa kihisia, kimwili, kingono na kutokuwa na uhakika wa malazi.*

*Kadhalika, uwepo wa mawasiliano ya wazi kati ya wazazi na watoto ni muhimu sana. Wazazi wanapaswa kujaribu kuelewa hisia na changamoto za watoto wao pamoja na kuwapa fursa ya kujieleza kuhusu hisia zao na masuala yanayowakabili. Kupitia mazungumzo ya wazi, watoto wanaweza kujifunza kuhusu madhara ya dawa za kulevya na jinsi ya kuziepuka.*

*Aidha, kutoa elimu kwa watoto kuhusu madhara ya dawa za kulevya inaweza kuongeza ufahamu wa mtoto na kumfanya aweze kufanya maamuzi bora. Watoto wanapaswa kuelewa madhara ya muda mrefu ya matumizi ya dawa za kulevya na jinsi yanavyoweza kuathiri ndoto zao za baadaye. Vilevile wazazi na walezi wanawajibu wa kuwasaidia watoto kuwa na vitu vya kujishughulisha navyo wakati wakiwa huru kama vile michezo, sanaa, na kazi za kujitolea ili kuwaongezea thamani na kuwapunguzia nafasi ya kutamani kujaribu dawa za kulevya.*

*Wakati mwingine watoto hukabiliwa na shinikizo rika au marafiki kuwafanya watumie dawa za kulevya .Hivyo, ni muhimu wazazi kuwasaidia watoto kutambua shinikizo hili na kutoa mbinu za kukabiliana nalo ikiwa ni pamoja na kuwafundisha jinsi ya kuchagua marafiki watakaowasaidia kufikia malengo yao. Ikiwa mzazi/ mlezi anawasiwasi au amethibitisha mtoto wake anatumia dawa za kulevya au kuhusika katika biashara ya dawa za kulevya, ni muhimu atafute namna ya kumsaidia.*

*Malezi bora ni darasa muhimu katika kujenga Taifa, lenye kizazi kisichotumia wala kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Hivyo, endapo kila mzazi/mlezi atatimiza wajibu kikamirifu atasaidia ustawi wa jamii katika nyanja zote.*

*Aretas Lyimo*
***Kamishna Jenerali***

Picha ya Jarida



*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan*

**Jarida hili limeandaliwa na**
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
*Aretas J. Lyimo*
***Kamishna Jenerali***

**Katibu**
*Florence B. Khambi*
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano***

**Wajumbe**
*Dkt. Peter P. Mfisi*
*Salmin K. Shelimoh*
*Moza K. Makumbuli*
*Ziliwa P. Machibya*
*Christina G. Rweshabura*
*Upendo K. Chenya*
*Daniel M. Kasokola*
*Seleman M. Edward*
*Lilian B. Matho*

**SHUKRANI**

*Mussa Ngarango Jr.*
***Mchora Katuni***

*Haji Abeid*
***Msanifu na Mchora Katuni***

# *Turudi Katika Tamaduni Zetu*



*MAMLAKA ya Kudhibiti Kupambana na Dawa za Kulevya hivi karibuni, ilikamata watu waliokuwa wakitengeneza biskuti zilizochanganywa na dawa ya kulevya aina ya bangi eneo la Kawe jijini Dar es Salaam. Hii si mara ya kwanza kukamatwa vyakula vilivyochanganywa na dawa za kulevya, kwani siku za nyuma katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kuliwahi kukamatwa watu wanaojihusisha na uhalifu wa aina hii. Tafsiri ya uhalifu huu ni kuwa, tatizo la dawa za kulevya limechukua sura mpya.*

*Pamoja na jitihada ambazo wazazi wamekuwa wakielekezwa kuweka mkazo katika malezi ya watoto, wahalifu wa dawa za kulevya nao wanabuni mbinu mpya za jinsi ya kuwarubuni watoto na vijana kuingia katika matumizi na biashara ya dawa za kulevya.*

*Moja ya mbinu inayotumiwa na wahalifu wa dawa za kulevya ni kuchanganya dawa hizo kwenye vyakula hasa vile vinavyopendwa na watoto na vijana. Hii ni hatari nyingine inayotakiwa kutupiwa jicho la kipekee. Lengo la wahalifu hawa ni kurahisisha uuzaji wa dawa hizo kwa kificho pamoja na kuongeza idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya.*

*Pamoja na mabadiliko ya kijamii yalisababishwa na utandawazi na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano bado ni jukumu la jamii nzima kumlinda mtoto kama wahenga wasemavyo* ***"mtoto wa mwenzio ni wako".*** *Katika kutekeleza jukumu hili, jamii inapaswa irudi katika tamaduni zetu ya kwamba suala la malezi ni la kijamii na sio la mzazi peke yake.*

*Matumizi ya simu za mkononi yasiyodhibitiwa kwa watoto, michezo ya watoto, vipindi vya runinga ambayo haviendani na maadili na tamaduni za kitanzania na upendo uliopitiliza wa wazazi kwa watoto wao, umepoka umakini wa wazazi katika kufuatilia nyendo zisizofaa kwa watoto hivyo kuwapa uhuru uliopitiliza.*

*Pamoja na umuhimu wa teknolojia, bado jamii inawajibu wa kutazama, kuchukua au kubeba mambo yenye tija kwa kuwaelekeza watoto namna ya kutumia teknolojia hiyo kwa faida na kutupilia mbali mambo yasiyofaa.*

*Florence Khambi*
***Mhariri***

# 'Wazazi Fuatilieni Mienendo ya Watoto Wenu' - Rais Dkt. Samia.

Na Mwandishi wetu

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka wazazi na walezi nchini kusimamia vema malezi ya watoto wao ili kuwakinga na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Rais Samia alizungumza hayo tarehe 25 Juni, 2023 jijini Arusha wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya.

Alisema kuwa, mbali na juhudi zinazofanywa na serikali bado familia ina nafasi maalumu katika kudhibiti dawa za kulevya kwani wazazi na walezi wanaposhindwa kufuatilizia mienendo ya watoto wao na kuchukua hatua kila wanapogundua mabadiliko ya kitabia, ndipo watoto hao huweza kupotea na kusababisha mateso katika familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

"Niwakumbushe wazazi na walezi wenzangu tuchukue nafasi zetu katika kuhakikisha watoto wetu wanakwenda katika njia iliyonyooka. Kina mama tuwe wepesi sana kufuatilia nyendo za watoto wetu zaidi ya hapo wale tunaowaita watoto wa mtaani miongoni mwao wana baba na mama zao lakini wanatoroka majumbani kutokana na yanayotokea majumbani kwao, kati yao wengi huathirika na dawa za kulevya, na hii inatokana na kutokuwajibika kwa wazazi na walezi wao" amesema Mhe. Dkt. Samia.

Aidha, ameongeza kuwa janga la dawa za kulevya halichagui familia ya kuingia kwani familia nyingi zimeguswa kwa namna moja au nyingine na janga hilo bila kuangalia hadhi ya familia. Hivyo, mchango wa kila mtu unahitajika kuhakikisha tunajenga jamii iliyo salama na Taifa huru bila matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

"Niwakumbushe wazazi na walezi wenzangu tuchukue nafasi zetu katika kuhakikisha watoto wetu wanakwenda katika njia iliyonyooka."

*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan*

"Kuna msemo wa waswahili unaosema, kichaa huchekesha akiwa si ndugu yako, akipita kichaa anafanya vituko utacheka kwa sababu si ndugu yako lakini akiwa ndugu yako moyo unakuuma hutacheka. Sisi kama watanzania tumeacha kuchekana kwa sababu balaa hili limekumba watu wote katika jamii bila kubagua, hakuna jamii moja inayoweza kucheka jamii nyingine kwa sababu watoto wetu wote sasa wapo humo katika hilo janga" amesema Dkt. Samia.

Pamoja na hayo, Rais Samia alisema amefurahishwa na kauli mbiu ya mwaka huu inayosema "Zingatia Utu Boresha Huduma za Kinga na Tiba" kwani kauli mbiu hii inataka kila mmoja ajipime katika nafasi yake kuona ni jinsi gani anaweza kushiriki katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya.

Mhe. Rais aliwasisitiza vijana kushiriki katika kuijenga kesho yao kwa kujilinda dhidi ya vitendo visivyofaa ili kujitengenezea maendeleo yao ya kesho kwani juhudi za serikali peke yake hazitafua dafu ikiwa vijana hawatajilinda. Aliongeza kuwa, serikali inampango mkubwa kwa ajili ya vijana unaoitwa "Tuwajengee vijana kesho iliyo njema wenye lengo la kuwaweka vijana kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo kilimo na uvuvi pamoja na kuwatayarisha wawe na mafunzo ya amali ili waweze kujiajiri na kuajiriwa.





KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambanana Dawa za Kulevya Aretas Lyimo akishiriki kuteketeza mirungi katika operesheni tokomeza mirungi iliyofanyika Same, Kilimanjaro.

# Aretas Lyimo Hapoi Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

Na Mwandishi wetu

*"SHUKRANI za kipekee nikupe Lyimo, Aah ..Aretas Lyimo. Mheshimiwa, huyu mtu ndani ya muda mfupi ameleta matokeo chanya na makubwa kwenye nchi hii… Kamishna Jenerali wa dawa za kulevya.. ndio Kamishna wa kwanza nimeweza kumsikia akitambuliwa kwa kazi yake bora na nzuri na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba anafanya kazi inayoonekana. Mheshimiwa, Lyimo ndani ya wiki tatu amekamata magunia 5,465 ya bangi kavu na 578 ya bangi mbichi na heroin kilogram 205 katika mikoa minne ya Dar es salaam, Pwani, Kilimanjaro na Arusha".*

Nukuu hii ni ya msanii wa kughani mashairi nchini, Mrisho Mpoto iliyobeba usemi wa vijana wa kisasa wa **"Apewe maua yake".** Alisema haya kuakisi utendaji kazi wa Kamishna Jenerali Aretas Lyimo.

Tangu kuteuliwa kwake tarehe 16 Machi, 2023 hadi sasa amefanya kazi inayostahili pongezi katika maeneo mbalimbali hasa katika kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa hizo na kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya kwa kufanya operesheni kadhaa ambazo zimekuwa na matokeo chanya pamoja na kuja na mbinu shirikishi katika kuongeza mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

> "Mheshimiwa, Lyimo ndani ya wiki tatu amekamata magunia 5,465 ya bangi kavu na 578 ya bangi mbichi na heroin kilogram 205."
>
> *Mrisho Mpoto*



Hadi sasa operesheni hizi zimefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Mara. Katika mikoa hii Mamlaka chini ya uongozi wa Aretas Lyimo ilifanikisha ukamataji kilo 1,624,544, gunia 50 za mbegu za bangi na kuteketeza jumla ya ekari 2,816.5 za mashamba ya bangi na mirungi pamoja na mililita 3,840 za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Pethidine. Aidha, kwa kushirikiana na Bodi ya Kimataifa ya Kuzuia Dawa za Kulevya (INCB), Mamlaka imefanikiwa kuzuia kuingia

*Inaendelea Ukurasa wa 4*

# Lyimo Hapoi Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

*Inatoka Ukurasa wa 3*

nchini jumla ya tani 1.5 za kemikali bashirifu ambazo zingeweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya.

## "Arusha hatutaki bangi"

Katika vijiji vya Kisimiri juu na Lesinoni wilaya ya Arumeru na kijiji cha Lenglong wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Kamishna Lyimo aliongoza operesheni na kukamata jumla ya magunia 931 ya bangi kavu iliyokuwa tayari kuingia sokoni, ekari 953 za mashamba ya bangi ziliteketezwa.



*ASKARI wa JKT wakikusanya bangi iliyofekwa tayari kwa kuteketezwa.*


## Operesheni tokomeza mirungi Kilimanjaro yatikisa

Jumla ya ekari 535 za mashamba ya mirungi ziliteketezwa katika operesheni maalum katika vijiji vya Rikweni, Heikondi, Tae na Mahande, wilayani Same, Mkoa wa Kilimanjaro.


Operesheni hii imekuwa na matokeo chanya baada ya wananchi kwa hiari yao kuamua kuteketeza mashamba na kung`oa visiki vya mirungi katika maeneo yao pamoja na kujikita katika kilimo cha mazao mengine mbadala ya biashara.

## Bangi chanzo uharibifu wa mazingira Moro.

Mkoani Morogoro, operesheni ya siku nane ilifanyika katika wilaya za Morogoro mjini, Morogoro vijijini na Mvomero na kukamata jumla ya magunia 131 za bangi kavu iliyokuwa tayari kusafirishwa, kilo 120 za mbegu za bangi na kuteketeza jumla ya ekari 489 za mashamba ya aina hiyo ya dawa za kulevya zilizokuwa zimelimwa pembezoni kwa mto Mgeta.



*BAADHI ya askari wakifanya maandalizi ya kuteketeza bangi ilioyokamatwa eneo Kisaki Morogoro.*



*ZOEZI la uteketezaji bangi likiendelea Mkoani Morogoro.*

## Mikakati kabambe katika Uelimishaji

Mamlaka imetoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa kuwahusisha wanajamii hususan wale wenye ushawishi mkubwa kama vile viongozi wa dini, kimila, pamoja na viongozi wa Serikali za mitaa. Mbinu hizi zimeleta matokeo chanya kwa kiasi kikubwa na kupelekea wananjamii wenyewe kuchukua hatua stahiki katika kutokomeza kilimo, matumizi na



*KIONGOZI wa jamii ya Maasai akizungumza na wananchi wakati wa utoaji elimu uliofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kijiji cha Kisimiri Juu.*

*Inaendelea Ukurasa wa 5*

# Lyimo Hapoi Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

biashara ya dawa za kulevya hapa nchini

iongozi mkuu wa kimila wa jamii ya wamasai Tanzania (Laigwani Mkuu) Ole Kisongo nchini aliwaonya wananchi wa kisimiri juu wanaojihusisha na kilimo cha bangi na kuwataka kila mmoja kuwa mlinzi wa mwenzie.

"Ni laana, kutengeneza kitu kinachoweza kuua mtoto wako. Nimepiga marufuku kiongozi aina yoyote ndani ya jamii ya maasai kumuwekea dhamana mtu yeyote katika jamii hii aliyekamatwa na dawa za kulevya. Ukijihusisha na kilimo cha bangi kwa namna yoyote ile tutakuunganisha na vyombo vya dola uwajibishwe kisheria".



*KAMISHNA Jenerali, Aretas Lyimo (wa pili kushoto) akitoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya dawa za kulevya katika kijiji cha Kisimiri Juu.*


## Mtandao wa dawa za kulevya wavunjwa Iringa

Mamlaka, ilifanya operesheni maalum mkoani Iringa na kufanikiwa kukamata jumla ya kilo 276 za dawa za kulevya aina heroin na bangi operesheni hiyo ilifanyika katika Manispaa ya Iringa, na maeneo ya mpaka kati ya wilaya ya Kilolo, na Mpwapwa. Katika operesheni hiyo vinara wa biashara ya dawa za kulevya walitiwa nguvuni.

## Wakulima wa bangi bonde la mto Mara wafikiwa

Katika wilaya ya Tarime Rorya kwenye bonde la mto Mara, Mamlaka ilifanikisha kuteketeza jumla ya ekari 807 za mashamba ya bangi, ukamataji wa gunia 507 za bangi kavu iliyo tayari kusafirishwa, gunia 50 za mbegu za bangi pamoja na kuteketeza viwanda viwili vidogo vilivyokuwa vikitumika kuchakata na kufunga bangi kabla ya kusafirishwa.

Aidha, baadhi ya mambo yaliyobainika ni wakazi wa maeneo hayo kulifanya bonde la mto Mara kama eneo maalum kwa ajili ya kilimo cha bangi na kujimilikisha kwa kutoruhusu mtu yeyote asiye mkazi kuingia kwenye bonde kama sehemu ya



*SEHEMU ya Bonde la Mto Mara ambayo yalibainika mashamba ya bangi.*

kuficha uharifu wao.


Kadhalika, baadhi ya viongozi wa serikali ya vijiji vinavyopakana na bonde hilo wasiowaaminifu wamekuwa wakikodisha na kuuza mashamba kwa ajili ya kulima bangi ndani ya hifadhi ya bonde hilo.

## Biskuti za bangi zanaswa Dar es Salaam

Aidha, Mamlaka imekamata watu wanaojihusisha na utengenezaji wa biskuti kwa kuchanganya na skanka katika eneo la Kawe jijini Dar es salaam. Katika tukio hilo, watuhumiwa waliokamatwa kuendelea na uzalishaji wa biskuti hizo kwa kutumia mtambo mdogo wa kusaga skanka na vifaa vya kutengeneza biskuti za bangi. Vilevile, Mamlaka imebaini maeneo yanayotumika kama masoko ya kusambazia na kuuza skanka kwenye fukwe za Bahari ya Hindi.



Vita dhidi ya dawa za kulevya inahitaji viongozi shupavu na jasiri kama Kamishna Aretas Lyimo ambaye tangu kuteuliwa kwake amekuwa madhubuti katika kuongoza vita hii. Utendaji wake unatafsiri kwa vitendo matamanio ya serikali ya awamu ya sita ya kuwa na kizazi kisichojihusisha wala kushiriki kwenye biashara ya dawa za kulevya. Mara zote amekuwa akieleza wazi kwamba, watanzania wote tukizichukia dawa za kulevya na kushirikiana na Serikali ndani ya muda mfupi dawa za kulevya zitakuwa historia hapa nchini.






*KAMISHNA wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa CP Salum Hamduni wakisaini hati ya makubaliano kushirikiana katika kutoa elimu ya dawa za kulevya na rushwa kupitia klabu za TAKUKURU zilizopo katika shule na vyuo.*

# DCEA, TAKUKURU Zaunganisha Nguvu Kupinga Rushwa na Dawa za Kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wamesaini hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizi hususan katika kuzuia dawa za kulevya na vitendo vya rushwa hapa nchini kupitia vilabu vilivyopo katika shule za msingi, sekondari na vyuoni.

Makubalianao hayo yamesainiwa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo na Mkurugenzi wa TAKUKURU CP. Salum Hamduni, tarehe 26 Mei, 2023 katika ofisi ya TAKUKURU makao makuu jijini Dodoma.

Akizungumza mbele ya waandishi wa habari, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo amesema anafuraha kusaini MoU ambayo inawaunganisha TAKUKURU na DCEA katika kushirikiana kikazi kutoa elimu mashuleni na jamii kwa ujumla juu ya madhara ya dawa za kulevya na rushwa kwa jamii kwani makosa haya yanauhusiano wa karibu na yanahitaji suluhu ya pamoja.

> “Muungano huu ni muhimu kwani utasaidia kufanya matumizi sahihi ya rasilimali chache tulizonazo kutatua matatizo mawili kwa pamoja.”
> *Aretas Lyimo*

Amesema, “muungano huu ni muhimu kwani utasaidia kufanya matumizi sahihi ya rasilimali chache tulizonazo kutatua matatizo mawili kwa pamoja”

Pia amesema makosa yanayoshughulikiwa na Taasisi hizi mbili ni makosa ya kupangwa na vita dhidi ya makosa haya yanaupinzani kwenye jamii kwani yanaleta faida kwa wanayoyatekelezea hivyo kupitia ushirikiano huu na elimu itakayotolewa, vijana watajengewa hali ya uzalendo na kuijenga jamii kuchukia matendo ya rushwa na dawa za kulevya hivyo kuibua chachu ya maendeleo kwa Taifa.

Pamoja na hayo, kamishna jenerali Lyimo ameonesha nia ya dhati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupingana na rushwa na dawa za kulevya kwa kusema, “Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya dhati ya kuongoza jamii isiyo na rushwa wala dawa za kulevya, na kupitia makubaliano yaliyofanyika yataleta tija kwa jamii na kutimiza azma ya Mhe. Rais ya kuwa

*Inaendelea Ukurasa wa 7*

# DCEA, TAKUKURU

*Inatoka Ukurasa wa 6*

na jamii bora, ya wachapakazi, jamii ya wazalendo na jamii ya kulisukuma taifa mbele kupata maendeleo.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaahidi kushirikiana kikamilifu katika kuisimamia na kuimarisha vita dhidi ya rushwa na dawa za kulevya, na tutaendelea kushirikiana kuhakikisha jamii inaelewa madhara ya Rushwa na Dawa za kulevya. Tumeamua kuwekeza nguvu kubwa katika kuzuia kuliko kukamata maana kukamata kunakuja pale ambapo nguvu ya kuzuia imeshindikana. amesema kamishna jenerali Lyimo.

Naye CP. Salum Hamduni amesema, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupamban na Dawa za Kulevya na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wamekubaliana kutumia rasilimali walizonazo kuwahamasisha wanafunzi, vijana na jamii kwa ujumla kutoshiriki vitendo vya rushwa na biashara haramu ya dawa za kulevya pamoja na kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na mambo hayo.

"Tuna matarajio makubwa baaada ya kusaini makubaliano haya kwani nguvu yetu ya kudhibiti dawa za kulevya na rushwa itaongezeka na kufanya jamii ya watanzania kuwa salama" amesemA CP. HAMDUNI.

Aidha, amewaasa wanahabari kutumia vyombo vya habari kuunga mkono juhudi hizi kwa kuwahamasisha wananchi kushiriki katika kutokomeza vitendo vya rushwa na matumizi ya dawa za kulevya.

# Ushirikiano Kati ya DCEA na Vituo vya Forodha Kuongeza Kasi ya Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya




*KAMISHNA wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo alipowasili kituo cha forodha cha Tarakea Kilimanjaro kwa ajili ya kufanya kikao na baadhi ya watumishi ili kuimarisha juhudi za mapambano dhidi ya dawa za kulevya mipakani.*

**Na Mwandishi Wetu**

USAFIRISHAJI wa dawa za kulevya ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka. Katika kulitambua hilo, Serikali imeweka mkakati mahsusi wa kudhibiti changamoto hiyo katika vituo vyote vya forodha kwa kushirikiana na taasisi na mamlaka zinazofanya kazi katika vituo hivyo. Lengo ni kuimarisha ukaguzi wa mizigo na watu ili kudhibiti mianya ya kupitisha dawa za kulevya.

Dawa nyingi za kulevya husafirishwa na kuingizwa nchini kupitia mipaka ya nchi kavu na majini, hivyo imeonekana ni lazima kuimarisha mifumo ya ukaguzi wa mizigo na watu katika viwanja vya ndege, bandari na vivuko vyote vya watu na mizigo. Katika kufanikisha azma hiyo Mamlaka imetembelea vituo vyote vya forodha na kutoa elimu ya utambuzi na mbinu mbalimbali zinazotumika kuficha dawa za kulevya ili kukabiliana na changamoto zinazofifisha udhibiti wa dawa za kulevya. Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kuhakikisha changamoto zinazojitokeza zinatatuliwa ili kuongeza kasi ya udhibiti wa dawa za kulevya katika maeneo ya mipakani.

"Ushirikiano baina ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, taasisi nyingine na wananchi umeanza kuzaa matunda na tumefanikiwa kubaini mitandao ya wafanyabishara wa dawa za kulevya ambao walikamatwa kupitia operesheni endelevu za pamoja zinazofanyika mipakani", Kamishna Jenerali Lyimo amesema.

Ameongeza kuwa, ushirikiano huo umefanikisha ukamataji wa kilo 423.54 za bangi aina ya skanka zilizoingizwa nchini kupitia mipaka ya Tunduma na Rukwa zikitokea nchi za kusini mwa Afrika.

Ziara ya Kamishna Jenerali katika mipaka hiyo ililenga kujenga uelewa wa utambuzi wa dawa za kulevya, kuimarisha mahusiano na taasisi zilipo katika vituo na kutatua changamoto zinazovikabili vituo hivyo hasa katika ukaguzi wa watu na mizigo ili kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Sheria

# Mali za Mfanyabiashara wa Dawa za Kulevya Zataifishwa



Na Mwandishi Wetu

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imeridhia kutaifishwa kwa mali zilizokuwa zikimilikiwa na mfungwa Yanga Omary Yanga maarufu kama rais wa Tanga kufuatia Maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini dhidi ya mfungwa huyo kuomba mali zake zitaifishwe.

Uamuzi huo uliotokana na shauri namba 1/2021 uliotolewa na Jaji Elinaza Luvanda baada ya kuridhika pasipo shaka kuwa, mali za mshtakiwa huyo zinatokana na kosa la usafirishaji wa dawa za kulevya.

Mali zilizotaifishwa na Mahakama ni Kiwanja No, 32 Block “C” Magaoni Tanga, Kiwanja namba 73 Block “A” Mwambani Tanga, Kiwanja No. 144 Block “B” Mwakidila Tanga, kiwanja namba 615 na namba 617 Block “B” Kange Tanga, Kiwanja namba 30 Block “C” Mwakidila/Magoani Tanga, kiwanja namba 605 Block “A” Mwambani Tanga na kiwanja namba 606 Block “A” Mwambani Tanga.

Wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na wakili wa serikali Mwandamizi Sabrina Joshi na upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Nehemia Mkoko. Akisoma uamuzi huo Jaji Luvanda alisema sheria imeelekeza kuwa, mali zote zinazopatikana kwa njia ya uhalifu ni lazima zitaifishwe ili kutoa fundisho kwa jamii kuwa uhalifu haulipi.

> Mwaka 2020 mfungwa Yanga Omari Yanga alihukumiwa miaka 30 gerezani kwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin.



Mwaka 2020 mfungwa Yanga Omari Yanga alihukumiwa na Mahakama hiyo kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin.

## Sheria inasemaje ukitiwa hatiani kwa kosa la kufanya biashara ya dawa za kulevya?

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanaongozwa na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya Mwaka 2015. Chini ya Sheria hii, kujihusisha kwa namna yoyote ile na dawa za kulevya ikiwemo kilimo, matumizi, biashara ya dawa hizo, kumiliki vifaa, mitambo au mashine kwa lengo la kutengeneza dawa kulevya, kusaidia au kuwezesha ufanyaji wa biashara ya dawa za kulevya, kushikilia mtu kama dhamana kwa nia ya kufanya biashara ya dawa za kulevya, ni kosa la jinai.

## Adhabu kwa baadhi ya makosa ya kujihusisha na dawa za kulevya

### Kujihusisha na kilimo cha mazao haramu

Sheria inaharamisha mambo mbalimbali yanayohusiana na kilimo cha mazao haramu ikiwemo bangi, mirungi, kulima na

*Inaendelea Ukurasa wa 9*

Sheria

# Mali za Mfanyabiashara wa Dawa za Kulevya

*Inatoka Ukurasa wa 6*

kumiliki mbegu zinazoweza kuzalisha dawa za kulevya kwa kutoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 30. Mfano Damian Jankowski alipewa adhabu ya kifungo cha miaka 30 Jela baada ya kutiwa hatihani kwa kujihusisha na biashara na kilimo cha bangi.

### Kijihusisha na dawa za kulevya kwa mujibu wa kifungu cha 15A

Kutiwa hatiani kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya au kujihusisha isivyohalali na vitu vyenye madhara sawa na ya dawa za kulevya au zinazoweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya, zenye kiasi kilichoainishwa kwa mujibu wa kifungu cha 15A cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, adhabu yake ni kifungo miaka 30 jela.

### Kifungu hiki cha 15A kinahusu:

Kujihisisha na dawa za kulevya zenye uzito wa gramu 200 au chini yake; kemikali bashirifu au vitu vyenye madhara sawa na dawa za kulevya vyenye ujazo wa lita 100 au chini yake vikiwa katika hali ya kimiminika au vyenye uzito wa kilogramu 100 au chini yake vikiwa katika hali yabisi; au bangi au mirungi yenye uzito wa kilogramu 100 au chini yake, kemikali bashirifu au vitu vyenye madhara sawa na dawa za kulevya vyenye ujazo wa lita 100 au chini yake vikiwa katika hali ya kimiminika au vyenye uzito wa kilogramu 100 au chini yake vikiwa katika hali yabisi; au bangi au mirungi yenye uzito wa kilogramu 100 au chini yake.

### Kujihusisha na dawa za kulevya kwa mujibu wa kifungu cha 15

Kifungu cha 15 kinatoa adhabu ya kifungo cha maisha kwa kujihusisha na dawa za kulevya zaidi ya gramu 200, kemikali bashirifu au vitu vyenye madhara sawa na dawa za kulevya vyenye ujazo wa zaidi ya lita 100 katika hali ya vimiminika, au vyenye uzito wa zaidi ya kilogramu 100 vikiwa katika hali ya yabisi; au bangi au mirungi yenye uzito wa zaidi ya kilogramu 100; kemikali bashirifu au vitu vyenye madhara sawa na dawa za kulevya vyenye ujazo wa zaidi ya lita 100; vikiwa katika hali ya kimiminika au vyenye uzito wa zaidi ya kilogramu 100 katika hali yabisi; au bangi au mirungi yenye uzito wa zaidi ya kilogramu 100.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 15 kutiwa hatiani kwa kuwezesha au kusababisha mtu kushikiliwa kama dhamana kwa nia ya kufanya biashara ya dawa za kulevya adhabu yake ni kifungo cha maisha.

## Sheria inasemaje kuhusu kutaifisha mali za watuhumiwa wa dawa za kulevya?

Mali zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya ni mazalia ya uhalifu hivyo inabidi zitaifishwe ili kutoa funzo kwa wafanyabiashara .ya dawa za kulevya kuwa biashara ya dawa hizo hazilipi.

### Utaifishaji wa mali za watuhumiwa wa dawa za kulevya kwa mujibu wa kifungu cha 49

Mali zinazomilikiwa na mfanyanyabiashara wa dawa za kulevya au washirika wake kabla ya miaka 10 tangu aliposomewa mashtaka zinatakiwa kutaifishwa kuendana na utaratibu kama ulivyoainishwa chini ya Sheria ya Mazalia ya uhalifu.


### Utaifishaji huu unahusisha yafuatayo;

a) Mtu aliyetiwa hatiani kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
b) Mtu aliyetiwa hatiani na Mahakama nje ya nchi
c) Mshirika wa mtuhumiwa kama ilivyoainishwa kwenye kipengele a na b hapo juu.

Endapo mtu atakuwa na pingamizi kuhusiana na mali ya mazalia ya uhalifu iliyotaifishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, anaweza akawasilisha maombi kwenye Mahakama iliyotoa uamuzi kupinga uamuzi huo.



*SHAMBA la bangi la Jankowski lenye ukubwa wa ekari moja.*



*DAMIAN Jankowski raia wa Poland akielekea mahakamani kusikiliza shauri lake kabla ya hukumu yake.*



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo ya heshima kutambua mchango wake katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya iliyotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na kukabidhiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa.



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Aretas Lyimo kuwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya tarehe 19 Machi, 2023.



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu akisikiliza maelezo kuhusu shughuli zinazofanywa na Mamlaka kwenye Kilele cha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya iliyofanyika kitaifa tarehe 25, Juni 2023 jijini Arusha.



KAMISHNA jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa CP Salum Hamduni wakionesha hati ya makubaliano waliyosaini kushirikiana katika kutoa elimu ya dawa za kulevya na rushwa kupitia klabu za TAKUKURU zilizopo katika shule na vyuo.



KAMISHNA Jenerali Aretas Lyimo na wadau wengine walipotembelea kiwanja inapojengwa ofisi za DCEA makao makuu, Jedengwa, Dodoma.



VIONGOZI wa dini na kimila mkoani Arusha wakifuatilia hotuba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Taifa katika kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Dawa za kulevya Duniani.



KAMISHNA Aretas Lyimo akiwa kwenye picha ya pamoja na wadau kutoka taasisi za udhibiti na wawakilishi kutoka sekta binafsi kutoka katika viwanda vya kemikali na dawa tiba zenye asili ya kulevya baada ya tukio la utiaji saini wa hati ya ushirikiano katika udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.



BAADHI ya mbinu zinazotumiwa na waharifu wa dawa za kulevya kuficha dawa hizo kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji.

Shuhuda



*JUDITH Uloki akitoa ushuhuda katika kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya yaliyofanyika kitaifa jijini Arusha.*

# Judith: Sigara ya mpenzi iliniponza, sikujua nitaishia pabaya katika 'utumwa wa unga'

**Na Mwandishi Wetu**

NAITWA Judith Uloki, mzaliwa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Hai, Kijiji cha Uswaa Machame, nililelewa na bibi yangu baada ya wazazi wagu kutengana. Ni mraibu niliyepata nafuu baada ya kupatiwa matibabu kwa dawa ya methadone katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mount Meru – Arusha.

Nikiwa na umri wa miaka 20 nilifanikiwa kupata kazi saluni hivyo nilianza kujitegemea. Baada ya muda nilifanikiwa kufungua saluni yagu eneo la Moshono, Arusha. Na hapo ndipo nilikutana na mchumba wangu aliyeniingiza kwenye dawa za kulevya. Alinifundisha kuvuta sigara, ambazo alikuwa anachanganya na dawa za kulevya bila mimi kujua na hatimaye nami nikawa mtumiaji wa dawa hizo pasipo kujua.

Siku moja nilipata msiba nyumbani kwetu, ilinilazimu kwenda, siku ya kwanza nikiwa huko, niliamka vizuri, lakini siku ya pili niliamka kama vile mtu mwenye homa, viungo vyote vya mwili viliniuma kwa kifupi nilikuwa naumwa sana. Nilikwenda zahanati lakini nilipofanyiwa uchunguzi hakuna ugonjwa ulioonekana. Nilihisi labda zahanati zetu hazina huduma za kutosha, nilirudi Arusha na kwenda Mount Meru nako hawakuona ugonjwa wowote.

> "Alinifundisha kuvuta sigara, ambazo alikuwa anachanganya na dawa za kulevya bila mimi kujua,"
> *Judith Uloki*



Niliporejea nyumbani mume wangu aliponiona alishtuka kwa sababu aliona nina hali mbaya. Mume wangu aliniambia alijua tu, nilimuuliza, alijua nini? Aliniambia alijua kama naumwa na hajaambiwa na mtu, alinishauri nivute sigara nitakaa sawa. Nilimkatalia, siwezi kuvuta… kwani tangu imeingia ndani harufu ya sigara ilinifanya nizidi kujisikia vibaya lakini alinisihi nivute. Nilipovuta ghafla nilihisi nimepona.

Nilishangazwa sana na ile hali na kumuuliza mbona kama nilimekuwa mzima? mbona kama nimepona sisikii tena maumivu? Akaniambie eehe!! mama yangu, wewe saizi hutakiwa kukaa bila kukosa hii kitu tayari umeshapata arosto. Niliuliza arosto ya nini!? akaniambia hujui kama wewe unavuta unga? Hiyo ni dawa za kulevya. Nilishangaa, dawa za kulevya? eehee! alinijibu ndiyo, siku zote huwa nachanganya kwenye sigara tunazovuta.

Siku hiyo ndiyo nilijua kuwa nimetumia dawa za kulevya kwa muda wa miezi saba bila mimi kujua. Nilichukizwa na kitendo hicho, lakini ilikuwa tayari nimeshachelewa kwani nilitamani kuacha lakini kila nilipojaribu nilishindwa kutokana na maumivu makali niliyokuwa nikiyapata. Hivyo, nililazimika kuendelea kutumia dawa za

*Inaendelea Ukurasa wa 13*

## Sigara ya mpenzi iliniponza

*Inatoka Ukurasa wa 12*

kulevya kwa muda wa mwaka mmoja na miezi tisa.

Ili niweze kupata fedha za kununua unga, nililazimika kuuza vifaa vyote katika saluni yangu pamoja na vitu vya ndani na baadaye kuwa na maisha magumu zaidi. Nilianza kuwa mdokozi, niliiba vitu vya watu ilia pate pesa nikanunue dawa hizo haramu. Mbali na kuiba, pia tulikuwa tukikopa huku na kule na baada ya deni kuwa kubwa nyumba ya familia yangu ilipigwa mnada. Hivyo, nilijikuta nimepoteza nyumba ya urithi kwa sababu ya matumizi ya 'unga'.

Mbali na kutumia dawa za kulevya, pia tulijihusisha na uuzaji wa dawa hizo. Kwa kuwa nilikuwa na kiasi kikubwa cha heroin ndani, hivyo nilitumia zaidi hadi kufikia hatua ya kujidunga. Nilikuwa najichoma kete nne, baadae sita, nane hadi kumi na tano. Niliwahi kukamatwa nikiuza heroin na kufungwa jela, nikiwa huko nikajigundua ni mjamzito.

Baada ya kutoka jela, nilikutana na asasi ya YCR, walipokuwa wakipita majumbani kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kutumia dawa za kulevya. Awali niliwachukulia poa, hawakukata tamaa, waliendelea kuja na baadaye niliwaelewa na kunipa elimu ya unasihi na baada ya muda waliniunganisha kwenye matibabu ya methadone katika liniki ya Mount Meru.

Nashukuru kwa sasa naendelea vizuri na matibabu yangu na naiomba Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kuendelee kupanua huduma hii ili kuwafikia waraibu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pia naomba vijana walioacha dawa za kulevya waweze kuunganishwa/kupata fursa za ajira ili wajikwamue kimaisha na kufanya shughuli halali za kuwaingizia kipato.

# 'Tumeamua kubadilika, familia, jamii msitutenge' - Brown

**Na Mwandishi Wetu**

Ni miaka 40 sasa tangu Boss Brown alipozaliwa, ni msomi mwenye shahada ya mawasiliano aliyoipata kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino nchini Tanzania. Ndani ya kisa hiki anasimulia jinsi alivyojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.

''Mimi ni mwathirika wa vilevi na dawa za kulevya. Sababu zilizonifanya kuingia katika vilevi ni makundi niliyokuwa nayo wakati nikiwa kidato cha kwanza na changamoto nyingine za maisha".

Aliendelea kusema, ''matumizi ya dawa za kulevya yalisababisha uwezo wangu wa shule upungue hata nilivyohitimu sikupata ufaulu wa kiwango nilichokuwa nakihitaji".

Anasema alifanikiwa kupata kazi iliyoweza kumsaidia maisha yake lakini nayo aliipoteza. Dawa za kulevya zimemsababishia changamoto nyingi za kifamilia, aliwahi kupata msichana aliyemchumbia, walizaa mtoto mmoja lakini mwisho wa siku naye waliachana kwani hakuweza kukidhi mahitaji ya mtoto wake.

Baada ya hali kuwa mbaya, aliamua kwenda 'Sober House' kuanza tiba ili kuachana na utumwa wa dawa za kulevya.

"Nilikutana na rafiki yangu ambaye naye aliathiriwa na dawa za kulevya, aliponiona alisikitika sana, na kunishauri kwenda 'Sober House' au clinic {MAT}, nilikubaliana naye, niliweza kuanza tiba katika sober house iitwayo Muungano Recoverly Community (MRC) ambapo kwa na sasa naendelea vizuri," anasema.

Anaongeza kuwa, "kwa hali yangu, sasa nipo vizuri, namshukuru Mungu maisha yangu yanaendelea, afya yangu imeimarika na sasa naweza kufanya majukumu na kuweza kufikiria na kuwa na mipango endelevu katika maisha yangu".

Brown anawashauri ambao hawajaingia katika janga hili la ulevi na matumizi ya dawa za kulevya waweze kujifunza kwa kuwaona tu watu ambao wanaathirika jinsi wanavyoteseka, na mtu ambaye hajatumia ajue ana neema na aweze kuitunza.

"Kwa sababu utakapo ingia kwenye kutoka ni vigumu na utakuwa umepoteza vingi kwa hiyo mtu ambaye ujaingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya ujilinde sana pamoja na kujiepusha na makundi ambayo yana tabia hizi kwa sababu unaweza kupoteza dira ya maisha yako. Pia kwa watu wanaotumia wanaweza kujiunga na huduma za matibabu zinazopatika hapa nchini".

Ameshauri Serikali iendelee kuchukua hatua, kupambana na kudhibiti dawa hizo kwani ni tatizo kubwa na kuendelee kuwasaidia wale wanaotaka kubadilika.

Aidha, ametilia mkazo suala la elimu kwa jamii kuhusu athari za biashara na matumizi ya dawa hizo haramu ili wasijiingize huko. Pia familia zitambue na kukubali kuwa hili tatizo lipo na kuepuka unyanyapaa kwa waraibu ili kuwasidia kukamilisha safari yao ya utengamao.

"Upendo ni kitu kikubwa sana mtu anavyoingia katika tatizo hili ni kama tatizo lingine sisi huwa tunakosa upendo kwa familia tunatengwa, tunatukanwa. Tukumbuke familia ina mchango mkubwa, mtukaribishe katika familia, tumeteleza, tumeanguka, tumejirekebisha na sasa tunahitaji kupendwa na kurudi katika jamii".



Brown ameiomba serikali kuwawezesha waraibu waliopata nafuu kwa kuwaunganisha kwenye fursa za ajira na ujasiriamali ili wameze kujitegemea kiuchumi.

# Uraibu wa Bangi na Matibabu Yake

Na Mwandishi Wetu

BANGI ni aina ya dawa ya kulevya inayotokana na mmea unaoitwa "Cannabis sativa" ambao hulimwa na kutumika kwa wingi hapa nchini na maeneo mengi duniani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2023, inayoandaliwa na Shirika linaloshughulikia dawa za kulevya na Uhalifu (UNODC), bangi ndiyo dawa inayotumika zaidi Duniani. Inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 219 Duniani walitumia bangi mwaka 2022.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, asilimia 70 ya watumiaji wa bangi ni wanaume na asilimia 30 ni wanawake. Aidha, takribani watoto milioni 13.5 wenye umri wa ya miaka 15-16 walitajwa kutumia bangi kwa mwaka 2021. Kwa kuwa ubongo wa watoto unaendelea kukua, matumizi ya bangi yanaweza kusababisha uharibifu mkubwa kwenye mfumo wa fahamu.

Taarifa hiyo inaonesha kuwa asilimia 40 ya nchi zilizohalalisha kilimo cha bangi kwa ajili ya matumizi au kwa ajili ya kutengenezea dawa za tiba zimeripoti kuongezeka kwa magonjwa ya akili na uhalifu. Aidha, bangi ndiyo dawa iliyoripotiwa kusababisha idadi kubwa ya madhara/magonjwa yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kuliko dawa nyingine.

Pia, bangi ni moja ya chanzo cha matumizi ya dawa za kulevya za viwandani kama vile heroin, cocaine n.k. Hatua hii inapelekea idadi kubwa ya waraibu wa dawa za kulevya wanaopatiwa matibabu kutokana na matumizi ya dawa hizo ni watumiaji wa bangi. Hata hivyo, dawa inayosababisha madhara makubwa zaidi ikiwa ni pamoja na vifo ni Heroini.

## Matibabu ya Waraibu wa Bangi

Matibabu ya uraibu wa bangi huweza kupatikana katika idara za afya ya akili za hospitali za wilaya, mikoa na hospitali za rufaa za Kanda na katika nyumba maalumu za upataji nafuu (Sober Houses). Hadi sasa hakuna dawa iliyoidhinishwa Duniani inayotibu uraibu wa bangi.

## Matibabu ya Uraibu wa Bangi Hospitalini

Mara nyingi uraibu wa bangi huambatana na matatizo mengine ya kiafya yakiwemo afya ya akili. Mgonjwa anapofika hospitalini hufanyiwa uchunguzi wa matatizo mengine ya kiafya yanayomkabili, baada ya hapo mpango halisi wa matibabu yake hupangwa kulingana na matatizo aliyonayo.

Mraibu wa bangi anapokosa kutumia dawa hiyo kwa wakati hupatwa na arosto. Arosto ni dalili anazozipata mraibu wa dawa za kulevya pale dawa anayoitumia inapokwisha mwilini na kukosa kutumia dawa nyingine. Baadhi ya dalili hizi ni pamoja na maumivu makali ya mwili, kutoa jasho jingi, homa, hasira, kuwa na wasiwasi, kuharisha maumivu ya kichwa n.k.

Hivyo, mraibu wa bangi anapokuwa hospitali pamoja na matibabu ya magonjwa mengine yanayoambatana na uraibu wake, pia hupatiwa matibabu ya arosto kadri ya dalili anazozipata kupunguza adha anayoipata kwa kukosa kutumia dawa hiyo. Baadaye mraibu huendelea na ushauri nasaha unaolenga kumfundisha mbinu mbalimbali za kuachana na matumizi ya bangi na jinsi ya kujitambua na kuzikabili changamoto mbalimbali katika maisha.

## Matibabu ya Uraibu wa Bangi Katika Nyumba Maalumu za Upataji Nafuu. (Sober House)

Matibabu ya uraibu wa bangi katika nyumba maalumu za upataji nafuu, hufanyika kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu. Hatua hizi 12, zinamfanya mraibu kujitambua yeye na matatizo yake.

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, uraibu wa bangi huambatana na matatizo mengine ya kiafya. Kwa kulitambua hilo, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ilitengeneza Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Nyumba Maalumu za Upataji nafuu.

Kwa Mujibu wa Mwongozo huu, Waraibu wote wanaosajiliwa kwenye nyumba hizi, hupelekwa hospitalini kwanza kwa ajili ya kupima afya zao. Hivyo, kwa wale wenye matatizo mengine ya kiafya hupatiwa dawa au kuunganishwa na huduma mahsusi wanazozihitaji kulingana na matatizo waliyonayo kama vile Kifua Kikuu na VVU.

Baada ya hapo waraibu hupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo ushauri nasaha unaolenga kumfundisha mbinu za kuachana na matumizi ya bangi na jinsi ya kujitambua na kuzikabili changamoto mbalimbali katika maisha. Wanapokuwa kwenye nyumba hizi, waraibu pia hufundishwa kazi za mikono kama vile kilimo, ufundi selemala na kuchomelea vyuma. Mafunzo haya huwasaidia kujipatia kipato baada ya kumaliza matibabu yao.

Muda wa kukaa katika matibabu kwa waraibu wa bangi hutofautiana kulingana na kiwango cha athari alizozipata mraibu. Inapendekezwa kuwa mraibu akae kwenye matibabu angalau miaka miwili, hii ni kwa sababu uraibu ni ugonjwa sugu wenye tabia ya kujirudia rudia. Hivyo, mraibu akikaa muda mfupi kwenye matibabu anakuwa na uwezekano mkubwa wa kurejea kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

## Hatua Kumi na Mbili za Narcotics Anonymous (Usitiri wa Mihadharati)

1. **Tulikiri ya kwamba hatukuwa na nguvu yoyote kuushinda uraibu, na kwamba tulishindwa kuyamudu maisha yetu.**
2. **Tulikuja kuamini kuwa nguvu kubwa zaidi kuliko sisi wenyewe ingeweza kuturudisha katika hali timamu.**

*Inaendelea Ukurasa wa 15*

# Ijue Methamphetamine

Na Mwandishi wetu

## Methamphetamine ni nini?

METHAMPHETAMINE ni dawa ya kulevya ambayo ipo katika kundi la vichangamshi **(Stimulants)** sawa na Cocaine, Amphetamine, Ecstasy n.k. Dawa hii kwa majina mengine hufahamika kama; *"Ice", "Crystal meth", "Speed", "Quartz" "Crystal glass"*.

## Mwonekano wa Methamphetamine





Mara nyingi, dawa hii inaweza kuwa kwenye mfumo wa vidonge, unga, au chembechembe mithili ya chumvi ang'avu yenye rangi mbalimbali.

## Chanzo cha Methamphetamine

Dawa ya methamphetamine huzalishwa kwa wingi kwenye maabara bubu (clandestine Laboratory) kutokana na kemikali bashirifu aina za ephedrine, pseudoephedrine na phenyl -2-propanone (P2P).

Kemikali aina ya ephedrine inaweza pia kuzalishwa kutoka kwenye mimea jamii ya *Ephedra sinica* ambayo inapatikana kwa wingi nchini Afghanistan.

## Matumizi na Madhara ya Methamphetamine?

Dawa hii inaweza kutumiwa kwa njia za kunusa, kuvuta, kujidunga na kumeza. Dawa hii hatari na yenye kiwango kikubwa cha kusababisha uraibu (addiction severity index) inaweza kusababisha madhara kwenye mfumo wa fahamu wa kati (Central Nervous System) na hivyo kuathiri afya ya akili.

Aidha, dawa hii inaweza kusababisha madhara ya muda mfupi na muda mrefu. Miongoni mwa madhara ya muda mfupi ni pamoja na kupoteza hamu ya kula, Kuongezeka kwa kasi ya mapigo ya moyo, kutetemeka, kifafa, kukosa usingizi na vifo vya ghafla. Madhara ya muda mrefu ni pamoja na kusababisha uraibu, kupata msongo wa mawazo, maumivu ya tumbo, kuchanganyikiwa, na kupoteza maisha.

## Udhibiti wa Methamphetamine

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya sura 95 imeainisha dawa hii kwenye jedwali la kwanza la dawa za Saikotropiki. Aidha dawa hii inadhibitiwa kimataifa kupitia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kudhibiti Dawa za Saikotropiki wa Mwaka 1971.

## Ukamataji wa methamphetamine hapa nchini

Tangu mwaka 2021 hadi 2022 Jumla ya kilo 431.74 zimekamatwa zikiingizwa nchini. Ukamataji huo ulihusisha raia wa Tanzania na Irani.

# Uraibu wa Bangi na Matibabu Yake

*Inatoka Ukurasa wa 14*

3. Tulikata shauri kukabidhi nia zetu na maisha yetu kwa ujali wa Mungu kama vile tulivyomfahamu.
4. Tulichunguza na kuorodhesha maadili yetu bila uoga.
5. Tulikiri kwa Mungu, kwetu binafsi, na kwa mtu mwingine, hulka kamili ya makosa yetu.
6. Tulikuwa tayari kabisa kumuachia Mungu atuondolee udhaifu wa tabia zetu.
7. Kwa unyenyekevu tulimuomba Yeye aondoe kasoro zetu.
8. Tuliandika orodha ya watu wote tuliowadhuru, na kuwa na nia ya kuwaomba msamaha.
9. Moja kwa moja tuliomba msamaha watu tuliowakosea na kufidia kila ilipowezekana, isipokuwa pale ambapo kufanya hivyo kungewadhuru wao au wengine.
10. Tuliendelea kujichunguza na kila tulipokosea tulikiri papo hapo
11. Tulitafuta kwa njia ya sala na kutafakari ili kuboresha mawasiliano yetu na Mungu kama tulivyomfahamu, tukiomba tuelewe nia yake kwetu sisi na uwezo wa kuitekeleza.
12. Baada ya kupata mwamko wa kiroho kutokana na hatua hizi tulijaribu kueneza ujumbe huu kwa waraibu, na kufuata kanuni hizi katika shughuli zetu zote.

# Wadau Wapewa Tuzo Ushiriki Vita ya Dawa za Kulevya

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliandaa tuzo kama ishara ya kuthamini mchango wa wadau mbalimbali wanaoshirikiana na Mamlaka katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Tuzo hizo zilitolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya siku ya kupiga vita dawa za kulevya mwaka 2023, yaliyofanyika kitaifa jijini Arusha.

Miongoni wa waliopokea tuzo hizo kutoka kwa Mhe. Rais ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, na Waziri wa nchi ofisi ya Waziri Mkuu (sera na uratibu) Mhe. Jenista Mhagama.



*MKURUGENZI wa Shirika la Gift of Hope Foundation Said Bandawe akipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*




*MWAKILISHI wa Ubalozi wa Uingereza Gordon McCracken akipokea Tuzo ya kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*OFISA Mshiriki wa DEA nchini, kutoka ubalozi ya Marekani Joe Vazquez akipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*MKURUGENZI Mkuu wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha Marekani (CDC) Dkt. Mahesh Swaminathan akipokea tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*MKURUGENZI Mkuu wa MDH Dkt. David Sando akipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Henry Joseph Foundation medical Research Institute (HJFMRI)Sally Chalamala akipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*NURU Salehe mmoja wa waanzilishi wa sober House akipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.*





*JUU: KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo akipokea tuzo baada ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuibuka mshindi wa pili katika kipengele cha Taarifa Bora za Mahesabu ya Fedha 2022/2023 kwa Taasisi za Serikali zinazojitegemea.*

*CHINI: VIONGOZI wa DCEA wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kupokea tuzo ya mshindi wa pili katika kipengele cha taarifa bora za mahesabu ya fedha 2022/2023 kwa Taasisi za Serikali zinazojitegemea.*

# DCEA Yang'ara Tuzo za Uandaaji Bora wa Taarifa za Mahesabu 2022

**Na Mwandishi Wetu**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imepata tuzo ya mshindi wa pili kwa Taasisi za serikali zinazojitegea zilizoandaa taarifa bora za mahesabu ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 ambazo hutolewa kila mwaka na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA).Tuzo hizo zilitolewa tarehe 01 Disemba, 2023 katika ukumbi wa APC ulioko Bunju jijini Dar es Salaam.

Baada ya kupokea tuzo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Aretas Lyimo alieleza kuwa, siri ya ushindi huo ni uaminifu katika matumizi ya fedha za Umma.

"Tuzo hii inadhihirisha jinsi gani Mamlaka ilivyo na uaminifu katika matumizi ya fedha za serikali, hii inashabihiana na uaminifu tulionao katika kufanya operesheni na kufanikiwa kuwakamata wafanyabishara wakubwa wa dawa za kulevya, ndiyo maana hata fedha za serikali tumeweza kuzitumia kwa uaminifu mkubwa pamoja na kuandaa taarifa bora za fedha na hatimaye kuibuka mshindi wa pili" alisema Kamishna Jenerali Lyimo.

Aidha, aliongeza kuwa, akiwa kama mtendaji mkuu wa Mamlaka atasimamia na kuhakikisha kuwa fedha za serikali zinazotokana na kodi za wananchi zinatumika kwa usahihi na kwa uaminifu mkubwa hali ambayo itasaidia utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha dawa za kulevya zinatokomezwa katika taifa letu.

Mshindi wa tuzo hizi hupatikana baada ya kukidhi vigezo vya kimataifa ambapo washiriki hutakiwa kuandaa taarifa za mahesabu yao kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa kwa Sekta za Umma (International Public Sector Accounting Standard - IPSAS) na Viwango vya Kimataifa kwa makampuni ya kifedha pamoja na mifuko ya kijamii (International Financial Reporting Standards - IFRS).

# Wadau wa Maendeleo Wanaoshirikiana na DCEA Katika Kuendesha Vituo vya MAT

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, imekuwa ikiratibu na kusimamia ujenzi na uendeshaji wa vituo vya MAT nchini. Vituo hivi vimeanzishwa katika maeneo yaliyoathirika zaidi na matumizi ya dawa za kulevya aina ya Heroin. Hadi sasa kuna vituo 15 hapa nchini, kati ya hivyo, vituo 11 ni vituo vikubwa (Mother Clinics) na vituo vinne ni vituo vidogo (Satellite Clinics).

Jiji la Dar es salaam linaongoza kuwa na vituo vingi vya MAT ambapo kuna vituo saba, kati ya hivyo vituo vitatu ni vikubwa na vituo vinne ni vidogo. Vituo vikubwa vipo katika hospitali za Muhimbili, Mwananyamala na Temeke, Vituo vidogo vipo katika vituo vya afya vya Vijibweni Kigamboni, Round Table Mbagala, Gereza la Segelea Segerea na Tegeta.

Vituo vingine vya MAT vipo katika mikoa ya Pwani vituo viwili, Mbeya kimoja, Songwe Kimoja, Dodoma kimoja, Mwanza kimoja, Tanga kimoja na Arusha kimoja. Ujenzi wa kituo cha Morogoro umekamilika na maandalizi ya ufunguzi wa kituo hiki yanaendelea.

> Vituo vidogo vinne vilivyoko katika mkoa wa Dar es salaam vilijengwa kwa msaada wa Mfuko wa Dunia wa kudhibiti Maralia, Kifua Kikuu na UKIMWI 'Global Fund.'

Wadau wa Maendeleo wamekuwa wakitoa mchango mkubwa katika ujenzi, uanzishaji na uendeshaji wa vituo hivi. Mathalani, ujenzi wa vituo vikubwa vya Dar es Salaam ulifadhiliwa na Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kudhibiti UKIMWI ***'U.S. President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR)'*** Kupitia Kituo cha Kudhibiti na kuzuia magonjwa cha Marekani ***Centers for Disease Control and Prevention (CDC).*** Vituo hivi vyote vitatu vinaendeshwa kwa ufadhili wa PEPFAR kupitia Shirika lisilo la Kiserikali la hapa nchini liitwalo Management and ***Development for Health (MDH)***

Vituo vidogo vinne vilivyoko katika mkoa wa Dar es salaam vilijengwa kwa msaada wa Mfuko wa Dunia wa kudhibiti Maralia, Kifua Kikuu na UKIMWI ***'Global Fund.'*** Vituo hivi vinaendeshwa na ***PEPFAR*** kupitia ***MDH***

Vituo viwili vilivyopo katika Mkoa wa Pwani vipo kwenye hospitali ya Mkoa wa pwani Tumbi na kingine kipo katika hospitali ya wilaya ya Bagamoyo. Ujenzi wa Vituo hivi vyote ulifadhiliwa na ***PEPFAR*** kupitia ***MDH.*** Uendeshaji wa vituo hivi hufanywa na PEPFAR kupitia shirika lisilo la kiserikali la kitanzania liitwalo *Tanzania Health Promotion Support (THPS)* na Mfuko wa Dunia wa kudhibiti Maralia, Kifua Kikuu na ***UKIMWI Global Fund.***

Vituo vya MAT vilivyoko Mbeya na Songwe vipo katika Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini na kile cha Songwe kipo katika Kituo cha afya cha Tunduma. Ujenzi wa vituo hivi ulifadhiliwa na ulifadhiliwa na Shirika la kimataifa la utafiti wa Tiba kutoka Marekani ***The Henry Jackson Foundation Medical research International (HJFMRI).*** Shirika hili hupata fedha kutoka idara ya ulinzi ya Marekani ***U.S Department of Defense (DoD).*** Uendeshaji wa vituo hivi hufanywa na ***HJFMRI.***

Ukarabati wa Kituo cha MAT Dodoma kilichopo eneo la Itega ulifanywa kwa msaada wa Global Fund. Kituo hiki kinaendeshwa na Hospitali ya Afya ya Akili mirembe kwa kushirikiana na ***Global Fund.***

Kituo cha MAT Kilichopo Mwanza kipo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure. Kituo hiki kilifanyiwa ukarabati na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Miradi ya Matibabu ya UKIMWI ***International Center for AIDS Care and Treatment Programs (ICAP)*** Shirika hili pia ndilo linaloendesha kituo hiki kwa kushirikiana na Hospitali ya Sekou Toure.

Kituo cha MAT cha Tanga kipo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo. Kituo hiki kilijengwa kwa msaada wa ***Global Fund*** na kinaendeshwa na Global Fund na Shika lisilokuwa la kiserikali la kitanzania ***Tanzania Health Promotion Support (THPS)*** ambalo linapata msaada kutoka ***PEPFAR*** na ***Global Fund.***

Kituo cha MAT cha Arusha kiko katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru. Kituo hiki kilijengwa kwa msaada kutoka ***Global Fund*** pia uendeshaji wa kituo hiki hufadhiliwa na ***Global Fund.***

Mamlaka inasimamia ujenzi wa kituo cha MAT cha Morogoro kinachojengwa katika eneo la Gereza la Kihonda mjini Morogoro. Ujenzi huu unaofadhiliwa na Global Fund uko katika hatua za mwisho na maandalizi ya kukifungua tayari yameshaanza.

Mfuko wa Dunia ***Global Fund*** pia unafadhiri ugawaji wa mabomba ya sindano kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga (***Needle and Syringe Program)*** ili kuwakinga wajidunga hao na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Mpango huu uko katika Mikoa ya Dar es salaamu, Pwani na Arusha.



*WAENDESHA mashtaka na wapelelezi mkoani Iringa wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kupata mafunzo juu ya uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya.*

# Wapelelezi na Waendesha Mashtaka wa Serikali Wajengewa Uwezo

**Na Mwandishi wetu**

WAPELELEZI na Waendesha Mashtaka wa Serikali wa mikoa ya Mara, Morogoro na Iringa wamekumbushwa kutumia weledi na kuzingatia taratibu za kisheria ili kuhakikisha mashauri ya dawa za kulevya yanamalizika katika hali ya kufanikiwa.

Hayo yameelezwa na Kamishna wa Huduma za Sheria wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bi. Veronica Matikila alipokuwa akiwasilisha mada juu ya upelelezi na uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya kwa kundi hilo katika mikoa husika.

Mafunzo haya yanafanyika kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, na Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa makosa ya Jinai kuhakikisha wanafanya mafunzo endelevu kwa Maafisa wanaopeleleza na wanaoendesha mashauri ya dawa za kulevya ili kukabiliana na changamoto za kiutendaji pamoja na kubadilishana uzoefu juu ya upelelezi na uendeshaji mashauri hayo.

Aidha, akizugumzia mafunzo hayo, Mkuu wa Mashtaka mkoa wa Mtwara Joseph Mauggo amesema, mwezi Juni mwaka 2023 Mheshimwa Waziri Mkuu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Kudhibiti Dawa za Kulevya aliekeza kuundwa kwa Tume ili kufanya tathmini ya mwenendo wa kesi za dawa za kulevya. Miongoni mwa mambo yaliyobainika na Tume hiyo ni kwamba Serikali inapoteza kesi nyingi. Moja ya sababu ni kutokuwa na uelewa wa pamoja wa watendaji muhimu kwenye masuala ya dawa za kulevya na ndio maana Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) zinashirikiana katika kuwawezesha waendesha Mashtaka na wapelelezi wa serikali ili kuziba mianya hiyo kwa kujenga uelewa wa pamoja jambo litakalo fanikisha kutatua changamoto na malalamiko ya wananchi na hatimaye jamii ione na kutambua jitihada zinazofanyika kwenye suala la dawa za kulevya.

Mada zilizowasilishwa na kujadiliwa ni pamoja na aina za ushahidi, namna ya kuthibitisha makosa ya dawa za kulevya na maeneo muhimu ya kuzingatia kwa waendesha mashtaka katika kuongoza upelelezi wa kesi za dawa za kulevya.

Kufanyika kwa mafunzo haya kwa waendesha mashtaka na wapelelezi hapa nchini, kutaongeza ufanisi kiutendaji hali ambayo itasaidia mashauri ya dawa za kulevya kutokaa kwa muda mrefu na badala yake kusikilizwa kwa wakati na kuharakisha upatikanaji wa haki kwa wahusika.

## Je, wajua?

### NEMBO YA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Maelezo ya kila sehemu ya Nembo na uhusiano wake na shughuli za Mamlaka

1. Jina la Taasisi
2. Ndege aina ya Tai akitumika kama ishara ya kuchunguza na kukamata
3. Kifupisho cha jina la Taasisi kwa lugha ya kiingereza

---

### MATUMIZI YA RANGI ZILIZOTUMIKA KATIKA NEMBO

- **Rangi ya kijani:**
  Rangi hii imetumika kuwakilisha mazao yote yanayodhibitiwa kwa mujibu wa sheria kama dawa za kulevya (mfano; bangi na mirungi).


- **Rangi ya blue:**
  Rangi hii imetumika kuwakilisha udhibiti wa eneo la bahari na maziwa ambayo ndio njia kuu ya upitishwaji na uingizwaji wa dawa za kulevya (heroin, cocaine, methamphetamine) hapa nchini.

- **Rangi ya njano:**
  Rangi hii imetumika kuwakilisha udhibiti wa matumizi ya kemikali bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya.

- **Rangi nyeusi:**
  Rangi hii imetumika kama kielelezo cha Utanzania thabiti unaopinga biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

## Katuni


MNAFAHAMU NINI KUHUSU ATHARI ZA DAWA ZA KULEVYA?
PIA ZINAHARIBU MATARAJIO MAZURI YA MAISHA YAKO YA SASA NA BAADAE
ZINAHARIBU AFYA YA AKILI
JAMANI DAWA ZA KULEVYA NI JANGA KWENYE JAMII YETU
TUKAE NA WATOTO WETU TUWAELIMISHE MADHARA YAKE
PIA TUTOE TAARIFA KWA MAMLAKA HUSIKA. TUSIWAFICHE WASAMBAZAJI NA WAUZAJI
©Musa NGARANGO JR
KITU PEKEE NINACHOTAKA KWAKO USOME! USIJE KUJIINGIZA KWENYE MAKUNDI YA WAHUNI NA WANAOTUMIA DAWA ZA KULEVYA
NAZINGATIA ELIMU BABA, MAANA HATA SHULENI TUMEFUNDISHWA ATHARI ZA DAWA ZA KULEVYA, NI MBAYA SANA
©Musa NGARANGO JR
MOB: 0765 389 398
MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA NI MABAYA SANA. HUYU ALIKUWA NA AKILI ZAKE KABISA SASA KAWA CHIZI
TUNAPOSEMA DAWA ZA KULEVYA NI MBAYA MAANA YAKE NI HII
KARIAKOO KARIAKOO HIYOOO!!


SEBENE
Na Haji Abeid
HADI MUDA HUU SIJAPATA HATA DALADALA MOJA NIPIGE DEBE NIPATE HELA YA UNGA
HALAFU HII KOFIA YA BABU YA KUFUMA HII... SIKOSI BUKU KUMI YA HARAKA!
NA UZEE HUO KUNIKAMATA LABDA UKATAMNBIKE
hajiabeid
LAANA WEWE NAKUKIMBIZA KIMYA KIMYA NIKUFUNZE ADABU
OOPS! LOH PUMZI ZISHAKATA!
hjabeid@gmail.com
MAMAAAAAAAAAH!
TWAA!
KUVUNJA BISKUTI HUWEZI NDIYO UNIWEZE MIMI?
UNGA UTANIUA... HATUA MBILI TU PUMZI KWISHA!

DRUG CONTROL AND ENFORCEMENT AUTHORITY · DCEA ·

SCAN ME

DIRA YETU: **Tanzania isiyojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.**

DHIMA YETU: **Kudhibiti na kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya kupitia mikakati ya kisekta kwa ajili ya ustawi wa taifa.**


Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana
na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327
Dar es Salaam

8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam

**Simu:** +255 22 211 3754/57
**Nukushi:** +255 22 211 3752
**Barua pepe:** cg@dcea.go.tz
info@dcea.go.tz

***Namba ya Mawasiliano Bila Malipo (Call Centre) 119***

@dceatanzania
@dceatanzania
@dcea tanzania
DCEATV
www.dcea.go.tz